**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 14 YA 2018 NA KUTUNGA SHERIA YA UWEKEZAJI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**UANZISHWAJI WA MAMLAKA**

4. Uanzishwaji wa Mamlaka.
5. Muhuri na nembo ya Mamlaka.
6. Kazi za Mamlaka.
7. Uwezo wa Mamlaka.
8. Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji.

**SEHEMU YA TATU**
**USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA**

9. Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.
10. Sifa za Mwenyekiti.
11. Katibu wa Bodi.
12. Kazi za Bodi.

13. Uwezo wa Bodi.

14. Mwenendo wa Bodi.

15. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

16. Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

17. Kukasimu uwezo na kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

18. Idara, divisheni na vitengo vya Mamlaka.

19. Wafanyakazi wa Mamlaka.


**SEHEMU YA NNE**
**UWEKEZAJI, CHETI CHA UWEKEZAJI NA VIVUTIO**


20. Nia ya kuwekeza.

21. Taratibu za maombi ya Cheti cha Uwekezaji.

22. Usitishaji na ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji.

23. Athari za ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji

24. Mtaji wa uwekezaji.

25. Hadhi ya Uwekezaji Mkakati.

26. Vivutio vya Uwekezaji.

27. Upatikanaji wa ardhi.

28. Uwekezaji wa teknolojia ya kisasa.

29. Uwekezaji katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

30. Uwekezaji uliotelekezwa.


**SEHEMU YA TANO**
**HAKI NA WAJIBU WA MAMLAKA NA WAWEKEZAJI**


31. Haki ya kusimamia uwekezaji.

32. Wajibu wa mwekezaji.

33. Ushirikishwaji wa wazawa na wajibu wa kijamii.

34. Haki ya kuhamisha faida, mapato na mishahara.

35. Dhamana ya Serikali juu ya ulinzi wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.

36. Ulinzi wa haki miliki ya ubunifu.

37. Ajira kwa Watanzania.

38. Ajira kwa wataalamu wa Kigeni.

**SEHEMU YA SITA**
**UTENGAJI WA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI**

39. Utengaji wa Maeneo Maalumu ya Uchumi.

40. Madhumuni ya Maeneo Maalumu ya Uchumi.

41. Kazi za Mamlaka katika Maeneo Maalumu ya Uchumi.

**SEHEMU YA SABA**
**MASHARTI YA FEDHA**

42. Vyanzo vya fedha na rasilimali za Mamlaka.

43. Bajeti ya Mamlaka.

44. Hesabu na Ukaguzi.

45. Akaunti ya Benki.

**SEHEMU YA NANE**
**MAKOSA NA ADHABU**

46. Makosa na adhabu.

47. Adhabu ya jumla.

48. Kumaliza kosa.

**SEHEMU YA TISA**
**MASHARTI MENGINEYO**

49. Kutambua makubaliano baina ya nchi mbili.

50. Kutunza siri.

51. Sifa na vivutio vya Mnunuzi.

52. Nyumba za biashara.

53. Daftari la Kumbukumbu.

54. Kampuni ya Uwendeshaji.

55. Uhaulishaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.

56. Huduma za kielektroniki.

57. Utatuzi wa migogoro.

58. Ada na tozo.

59. Marekebisho ya Jadweli.

60. Mapitio na Rufaa.

61. Kanuni.

62. Kufuta na kubakiza.

**JADWELI**

**SHERIA NAM. 10 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

1 Februari, **2024**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 14 YA 2018 NA KUTUNGA SHERIA YA UWEKEZAJI ZANZIBAR NA KUWEKA MASHARTI MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Uwekezaji Zanzibar, 2023 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.** Sheria hii itatumika kwa uwekezaji ambao umekidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, isipokuwa uwekezaji katika:

(a) utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi;

(b) makubaliano baina ya sekta ya umma na binafsi;

(c) ubia na Serikali;

(d) makubaliano ya uwekezaji na Serikali; au

(e) kemikali hatarishi, silaha za moto, silaha au miripuko.

Ufafanuzi.

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"ardhi" ina maana kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Umiliki wa Ardhi, Nam.12 ya 1992;

"Ardhi ya Akiba kwa Uwekezaji" maana yake ni eneo lililotengwa na Rais kuwa eneo la akiba kwa ajili ya shughuli za uwekezaji ikijumuisha visiwa vidogo vidogo;

"bidhaa kabla ya uendeshaji" inajumuisha kompyuta, samani, vipuri, vyombo vya moto, vyombo vya jikoni, zana na aina zote za bidhaa ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuanza uendeshaji wa mradi wowote ambavyo vitahitajika katika kipindi cha utekelezaji wa mradi;

"bidhaa za ujenzi" maana yake ni mitambo, mashine, vifaa, vifaa vya ujenzi, vyombo vya moto na bidhaa zote zinazohusiana na hizo ambazo ni muhimu kwa ajili ya ujenzi wa mradi katika kipindi cha utekelezaji;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 9(1) cha Sheria hii;

"Cheti cha Uwekezaji" maana yake ni cheti kilichotolewa kwa Mwekezaji na Mamlaka baada ya kukidhi masharti ya Sheria hii;

"Diaspora" ina maana kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Masuala ya Diaspora, Nam. 4 ya 2020;

"Kampuni" ina maana kama ilivyoelezwa chini ya Sheria ya Makampuni, Nam.15 ya 2013;

"kipindi cha utekelezaji" maana yake ni kipindi cha muda ulioanishwa katika Cheti cha Uwekezaji au kipindi chengine chochote kilichoidhinishwa na Mamlaka kwa ajili ya upangaji, usarifu, uwekaji, uendelezaji, uanzishaji, ujenzi, ukamilishaji au shughuli nyengine yoyote inayohusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa inayojumuisha kipindi kinachoanzia tarehe ya uidhinishaji wa mradi hadi kabla ya mradi kufunguliwa au kuanza uendeshaji;

"Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji" maana yake ni kituo kilichoainishwa chini ya masharti ya kifungu cha 8(1) cha Sheria hii;

"Maeneo Maalumu ya Uchumi" maana yake ni maeneo yaliyoainishwa chini ya kifungu cha 39(1) na (2) cha Sheria hii;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 4(1) cha Sheria hii;

"Mamlaka ya Forodha" maana yake ni eneo la kijiografia la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi nyengine yoyote mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini haijumuishi Maeneo Maalumu ya Uchumi;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 15(1) cha Sheria hii;

"mnunuzi" maana yake ni mtu ambaye amenunua na ana umiliki kamili wa nyumba kwa madhumuni ya makaazi ndani ya miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara ulioidhinishwa na Mamlaka;

"Mwekezaji" maana yake ni mwekezaji ambaye amepewa Cheti cha Uwekezaji kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mwekezaji Mzawa" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Zanzibar ambapo zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zake zinamilikiwa na Mtanzania;

"Mwekezaji wa Kigeni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa chini ya sheria za Zanzibar ambapo zaidi ya asilimia hamsini ya hisa zake zinamilikiwa na raia wa kigeni;

"Mwendelezaji" maana yake ni mwekezaji ambaye anajishughulisha na uendelezaji wa majengo au miundombinu kwa madhumuni ya kuuza au kukodisha majengo hayo chini ya masharti ya Sheria hii;

"mtaji" maana yake ni michango yote ya fedha taslimu, mitambo, mashine, vifaa, jengo na mali zozote za kibiashara zinazoweza kudumu zaidi ya miezi kumi na mbili tofauti na thamani ya mali za biashara ambazo hazitumiki katika shughuli za kawaida za biashara;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"uwekezaji" maana yake ni mtaji wa mwekezaji unaojumuisha uanzishaji au umiliki wa mali za biashara na inajumuisha utanuzi, urekebishaji, uimarishaji au ukarabati wa biashara;

"Uwekezaji Uliotelekezwa" maana yake ni uwekezaji wowote ambao umesita kufanya kazi zinazohusiana na shughuli zake za uwekezaji kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo;

"Uwekezaji Ulioidhinishwa" maana yake ni uwekezaji ulioidhinishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Uwekezaji Mkakati" maana yake ni Uwekezaji Ulioidhinishwa ambao umekidhi vigezo vilivyoanishwa chini ya masharti ya kifungu cha 25 cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na uwekezaji.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji wa Mamlaka.

**4**.-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na ufupisho wake itakuwa "ZIPA".

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri na kwa jina lake kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki au kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa, kukopesha fedha au kupokea ruzuku ya kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya kifedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo chochote au jambo ambalo kisheria linaweza kufanywa au kutekelezwa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Mamlaka.

**5**.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mamlaka katika nyaraka yoyote itathibitishwa na saini ya Mkurugenzi Mtendaji au afisa mwengine yeyote wa Mamlaka aliyeidhinishwa kwa maandishi na Mkurugenzi Mtendaji.

(3) Nyaraka yoyote inayokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mamlaka itawekwa muhuri wa Mamlaka na itathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Mamlaka.

**6.**-(1) Kazi za Mamlaka zitakuwa ni:

(a) kuweka mazingira mazuri ya kukuza, kuwezesha na kulinda uwekezaji;

(b) kuimarisha uwekezaji wenye ushindani;

(c) kuitangaza Zanzibar kuwa ni sehemu inayovutia kwa uwekezaji na biashara;

(d) kuainisha fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini pamoja na namna za kuwezesha upatikanaji wa fursa hizo kwa kushirikiana na mamlaka husika;

(e) kuibua na kufanya tafiti muhimu na kutumia matokeo ya tafiti hizo baada ya kupata idhini kutoka mamlaka husika;

(f) kufuatilia na kutathmini maendeleo ya Uwekezaji Ulioidhinishwa kila baada ya muda;

(g) kuhakikisha vivutio vilivyotolewa kwa Mwekezaji vinatumika katika miradi iliyokusudiwa na vinaendana na mpango wa biashara wa mwekezaji uliowasilishwa;

(h) kuanzisha, kuratibu na kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa shughuli za uwekezaji nchini;

(i) kusimamia, kudhibiti na kuendesha Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(j) kutunza daftari la kumbukumbu lililoanzishwa chini ya Sheria hii;

(k) kuwaunganisha wafanyabiashara wadogo wadogo, wadogo na wa kati katika fursa za uwekezaji;

(l) kutoa miongozo ya uchangiaji katika huduma za maendeleo ya kijamii;

(m) kuainisha na kupendekeza tozo, kodi na ada kwa huduma yoyote inayotolewa na Mamlaka;

(n) kuweka vigezo na viwango vya mtaji kwa ajili ya uidhinishaji wa miradi ya uwekezaji;

(o) kuishauri Serikali juu ya:

(i) sera na mikakati inayofaa inayohusiana na uwekezaji;

(ii) kupanga na kutekeleza mpango wa vivutio vya uwekezaji na kufuatilia matokeo yake; na

(iii) uwekezaji ambao ni muhimu kwa uchumi wa nchi; na

(p) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo inahusiana na kazi za Mamlaka.

(2) Mamlaka inaweza kumteua mwakilishi katika nchi yoyote kwa madhumuni ya kutekeleza kazi zake zozote iliyopewa chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Mamlaka.

**7**. Mamlaka itakuwa na uwezo wa:

(a) kutoa, kurekebisha au kufuta Cheti cha Uwekezaji kilichotolewa chini ya Sheria hii;

(b) kutoa amri, maelekezo, muongozo au toleo juu ya uwekezaji na mambo mengine yanayohusiana na hayo;

(c) kuomba taarifa kutoka kwa mtu yeyote ambapo Mamlaka ina sababu za kuamini kwamba mtu huyo ana uwezo wa kutoa taarifa, nyaraka au ushahidi unaoweza kuisaidia Mamlaka katika kutekeleza kazi zake;

(d) kuchunguza lalamiko lolote dhidi ya Mwekezaji au Uwekezaji Ulioidhinishwa;

(e) kukodisha ardhi na kutoa hati ya ardhi kwa Mwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(f) kuingia katika mradi wowote wa uwekezaji kwa kutoa taarifa au vyenginevyo kwa madhumuni ya utekelezaji wa kazi zake; na

(g) kuwekeza ndani au nje ya Zanzibar.

Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji.

**8**.-(1) Mamlaka itafanya kazi kama Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji kwa madhumuni ya kuwezesha utekelezaji wa kazi zake.

(2) Muundo, kazi na masharti mengine yanayohusiana na Kituo cha Huduma kwa Wawekezaji yataainishwa katika kanuni.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.

**9.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mtendaji;

(c) mjumbe mmoja kutoka:

(i) Wizara inayohusika na Fedha;

(ii) Wizara inayohusika na Biashara;

(iii) Kamisheni ya Ardhi;

(iv) Jumuiya ya Wafanyabiashara Zanzibar; na

(v) Mamlaka ya Mapato Tanzania.

(2) Wajumbe waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia jinsia.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe chini ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki, ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, uongozi, fedha, ujasiriamali au sheria kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Sifa za Mwenyekiti.

**10.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi, ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani yoyote inayohusiana na uwekezaji kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba katika nafasi ya uongozi; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**11**.-(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mfanyakazi wa Mamlaka atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi, ikiwa mfanyakazi huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka mitano katika utumishi wa umma; na

(c) uwezo mzuri wa mawasiliano.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na kwa kushauriana na Mwenyekiti:

(a) ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi kwa mujibu wa sheria.

Kazi za Bodi.

**12**. Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kuandaa, kufuatilia, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa sera na mikakati ya Mamlaka;

(b) kumshauri Waziri na taasisi nyengine za Serikali zinazohusika juu ya masuala yanayohusiana na sera ya uwekezaji na utawala;

(c) kuweka mikakati na sera zinazosimamia shughuli za Mamlaka;

(d) kuwasilisha ripoti za utekelezaji za robo mwaka na mwaka kwa Waziri; na

(e) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo inahusiana na kazi za Bodi.

Uwezo wa Bodi.

13.-(1) Uwezo wa Bodi utakuwa ni:

(a) kumuelekeza Mkurugenzi Mtendaji kuipatia Bodi taarifa, ripoti au nyaraka nyengine yoyote ambayo Bodi itaona ni muhimu kwa ajili ya kutekeleza kazi zake;

(b) kutoa maelekezo halali kwa Mkurugenzi Mtendaji kuhusiana na usimamizi, utendaji na sera za uendeshaji za Mamlaka;

(c) kuidhinisha:

(i) muundo wa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(ii) usajili na ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji;

(iii) bajeti ya mwaka ya Mamlaka;

(iv) Kanuni za Fedha, Kanuni za Utumishi na Mpango Kazi wa Mamlaka;

(d) kuajiri wafanyakazi wa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011;

(e) kusikiliza rufaa dhidi ya mfanyakazi wa Mamlaka; na

(f) kusimamia masuala ya kinidhamu kwa wafanyakazi wa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 na Kanuni za Utumishi za Mamlaka.

(2) Bodi inaweza kutoa maelekezo ya jumla ya kuiongoza Mamlaka.

Mwenendo wa Bodi.

14. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yataainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

15.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atawajibika kwa usimamizi wa utekelezaji wa kazi za kila siku za Mamlaka.

Sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

**16**. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji, ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya uchumi, usimamizi wa biashara, fedha, uongozi, uhusiano wa kimataifa, ujasiriamali au sheria kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kukasimu uwezo na kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

**17**. Mkurugenzi Mtendaji anaweza, kwa maandishi, kukasimu kazi au uwezo wake wowote kwa afisa yeyote wa Mamlaka, isipokuwa:

(a) utoaji na ufutaji wa hati ya ukodishaji wa ardhi katika Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(b) utoaji, urekebishaji na ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji;

(c) uwezo wa kumaliza kosa;

(d) utoaji wa miongozo au maelekezo ya uwekezaji; au

(e) uwasilishaji wa maombi ya vivutio vilivyoainishwa chini ya Sheria hii kwa mamlaka husika.

Idara, divisheni na vitengo vya Mamlaka.

**18**.-(1) Mamlaka itaanzisha idara, divisheni au vitengo kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo wataeuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu unaohusiana nazo.

(3) Wakuu wa idara na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

(4) Wakuu wa divisheni watawajibika kwa wakuu wa idara.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

**19**. Kutakuwa na wafanyakazi wa Mamlaka watakaoajiriwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## UWEKEZAJI, CHETI CHA UWEKEZAJI NA VIVUTIO

Nia ya kuwekeza.

**20**.-(1) Mgeni au Diaspora yeyote ambaye anakusudia kuwekeza au kufanya biashara Zanzibar atatakiwa kuomba Cheti cha Uwekezaji kwa Mamlaka.

(2) Mtanzania yeyote ambaye anakusudia kuwekeza au kufanya biashara Zanzibar anaweza kuomba Cheti cha Uwekezaji kwa Mamlaka.

Taratibu za maombi ya Cheti cha Uwekezaji.

**21**. Taratibu za maombi, masharti, utoaji, ada, uhalali, uhuishaji na marekebisho ya Cheti cha Uwekezaji yataelezwa katika kanuni.

Usitishaji na ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji.

**22**.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha Cheti cha Uwekezaji kilichotolewa chini ya Sheria hii, ikiwa Mamlaka ina sababu za kuamini kwamba:

(a) Cheti cha Uwekezaji kimepatikana kwa njia ya udanganyifu au upotoshaji;

(b) Mwekezaji akiwa katika hatua ya kuacha uwekezaji;

(c) Mwekezaji ameshindwa kuanza utekelezaji wa mradi wa uwekezaji ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe ya kupata nyaraka zote za kisheria zinazohitajika;

(d) mradi umetelekezwa;

(e) Mwekezaji ameomba vivutio ambavyo vimetolewa chini ya Sheria hii, kwa madhumuni mengine yasiyokuwa yale ambayo vivutio hivyo vimetolewa;

(f) Mwekezaji ameshindwa bila ya sababu za msingi kuanza shughuli za uwekezaji ndani ya muda uliowekwa ndani ya Cheti cha Uwekezaji; au

(g) Mwekezaji ameshindwa kutekeleza wajibu wowote uliowekwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka itatoa taarifa ya angalau siku thelathini kwa Mwekezaji kutoa sababu kwa nini Cheti chake cha Uwekezaji kisifutwe.

(3) Endapo Mwekezaji atatoa maelezo ya kuridhisha kwa Mamlaka, Mamlaka itaondosha zuio na kumuelekeza Mwekezaji kama itakavyoona inafaa.

(4) Mamlaka itafuta Cheti cha Uwekezaji endapo Mwekezaji:

(a) ameshindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki;

(b) ametoa maelezo yasioridhisha kwa Mamlaka; au

(c) ameuondoa Uwekezaji Ulioidhinishwa.

Athari za ufutaji wa Cheti cha Uwekezaji.

**23**. Endapo Mamlaka itafuta Cheti cha Uwekezaji kilichotolewa chini ya Sheria hii:

(a) uwekezaji unaohusiana na Cheti cha Uwekezaji utasita kuwa Uwekezaji Ulioidhinishwa;

(b) mkataba wa ukodishaji wa ardhi unaohusiana na Cheti cha Uwekezaji utafutika moja kwa moja; na

(c) vivutio chini ya kifungu cha 26 cha Sheria hii, vitasita na kodi yoyote iliyosamehewa italipwa ipasavyo.

Mtaji wa uwekezaji.

**24**. Maombi ya Cheti cha Uwekezaji yatazingatiwa endapo yamekidhi vigezo vilivyoainishwa chini ya Sehemu ya Kwanza ya Jadweli la Pili la Sheria hii.

Hadhi ya Uwekezaji Mkakati.

**25**.-(1) Mwekezaji anaweza kuomba hadhi ya Uwekezaji Mkakati kwa Uwekezaji wake Ulioidhinishwa kwa Mamlaka baada ya kutimiza vigezo vilivyoainishwa chini ya Sehemu ya Pili ya Jadweli la Pili la Sheria hii.

(2) Hadhi iliyoombwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatumika kwa Uwekezaji mmoja Ulioidhinishwa.

(3) Masharti yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatatambuliwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe ya kupatiwa hadhi hiyo.

Vivutio vya Uwekezaji.

**26**. Mwekezaji, pamoja na vivutio vilivyotolewa chini ya sheria za kodi za Zanzibar na sheria za Tanzania zinazotumika Zanzibar, atastahiki vivutio vya uwekezaji kama vilivyoainishwa katika Majadweli yanayohusiana na vivutio chini ya Sheria hii.

Upatikanaji wa ardhi.

**27**.-(1) Mamlaka, kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa chini ya Sheria hii, itatoa ukodishwaji wa ardhi kwa Mwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi.

(2) Endapo Mwekezaji atahitaji ardhi nje ya Maeneo Maalumu ya Uchumi, Mamlaka itawezesha upatikanaji wa ukodishwaji wa ardhi hiyo kupitia Waziri anayehusika na ardhi.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mwekezaji atamlipa fidia inayoendana na kwa wakati mtu anayekaa katika ardhi hiyo iliyokodishwa kwa mujibu wa kifungu hiki kutokana na maendeleo aliyoyafanya au faida inayotokana na ardhi hiyo.

(4) Fidia iliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, italipwa kabla ya ukodishwaji wa ardhi haujatolewa.

Uwekezaji wa teknolojia ya kisasa.

**28**. Mamlaka itatoa vivutio maalumu kuvutia uwekezaji wa teknolojia ya kisasa ikiwa ni ajenda ya kitaifa ambavyo vitaainishwa katika kanuni.

Uwekezaji katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

**29**. Mamlaka itatoa vivutio maalumu kuvutia miradi ya uwekezaji ya uchumi wa buluu ikiwa ni ajenda ya kitaifa ambavyo vitaainishwa katika kanuni.

Uwekezaji uliote-lekezwa.

**30**.-(1) Uwekezaji Ulioidhinishwa utachukuliwa kuwa umetelekezwa iwapo:

(a) mwekezaji au mtu aliyeachiwa dhamana ya kusimamia uwekezaji huo hayupo katika udhibiti halisi wa uwekezaji huo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo; au

(b) hakuna maendeleo yoyote yanayofanyika baada ya kumaliza kipindi cha miaka mitatu iliyotolewa na Mamlaka kwa ajili ya utekelezaji wa uwekezaji huo.

(2) Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, endapo Mamlaka itajiridhisha kwamba, uwekezaji umetelekezwa, Mamlaka inaweza:

(a) kufuta Cheti cha Uwekezaji kinachohusiana na uwekezaji huo;

(b) kutangaza mradi huo umetelekezwa kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti;

(c) kuchukuwa usimamizi wa Uwekezaji au mali iliyotelekezwa;

(d) kusitisha huduma zote za uwekezaji huo; na

(e) kupiga mnada uwekezaji uliotelekezwa endapo itawezekana kufanya hivyo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mwekezaji ambaye uwekezaji wake umetelekezwa hatolipwa fidia.

## SEHEMU YA TANO
## HAKI NA WAJIBU WA MAMLAKA NA WAWEKEZAJI

Haki ya kusimamia Uwekezaji.

**31**. Mamlaka itakuwa na haki ya kutumia njia zote muhimu katika kusimamia Uwekezaji ili kuhakikisha kwamba, shughuli zote za Uwekezaji zinafanyika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa ya Sheria hii.

Wajibu wa Mwekezaji.

**32**. Mwekezaji:

(a) atafuata sheria za Zanzibar na sheria za Tanzania zinazotumika Zanzibar;

(b) atawasilisha kwa wakati taarifa zinazohitajika kwa taasisi za Serikali zinazoshughulika na uwekezaji ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi zao;

(c) atafanya shughuli za uwekezaji kwa namna ambayo itawalinda watumiaji, mazingira, usawa wa kijinsia na kukuza ujuzi kwa wafanyakazi wake;

(d) atafuata miongozo na maelekezo ya ushirikishwaji wa wazawa na wajibu wa kijamii kutoka sekta husika;

(e) atawasilisha ripoti za robo mwaka na mwaka kwa Mamlaka zinazohusiana na utekelezaji na maendeleo ya uwekezaji wao;

(f) atatekeleza shughuli za uwekezaji kwa mujibu wa mpango wa biashara na mpango wa utekelezaji ulioidhinishwa na Mamlaka;

(g) ataruhusu afisa wa Mamlaka kutekeleza kazi na wajibu wao kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii; na

(h) atasajili mkopo wa nje katika Benki Kuu ya Tanzania.

Ushirikishwaji wa wazawa na wajibu wa kijamii.

**33.** Mwekezaji atafuata miongozo ya mazingira, jamii na utawala iliyotolewa chini ya masharti ya Sheria hii.

Haki ya kuhamisha faida, mapato na mishahara.

**34.**-(1) Mwekezaji wa Kigeni anaweza, baada ya kulipa kodi na madeni yote, kuhaulisha fedha nje ya Zanzibar kwa kutumia fedha za kigeni zinazobadilishika kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha vilivyopo:

(a) gawio linalotokana na uwekezaji au nje ya Uwekezaji wake Ulioidhinishwa;

(b) mtaji na riba zinazotokana na mkopo wowote wa nje unaohusiana na Uwekezaji wowote Ulioidhinishwa Zanzibar; na

(c) mapato yanayotokana na ufilisi au mauzo ya Uwekezaji Ulioidhinishwa.

(2) Mtaalamu aliyeajiriwa na Mwekezaji anaweza kuhamisha, mshahara na malipo mengine aliyoyapata kutokana na ajira yake kwa kutumia fedha za kigeni zinazobadilishika kwa viwango vya ubadilishaji wa fedha vilivyopo kwa mujibu wa sheria zinazohusika.

Dhamana ya Serikali juu ya ulinzi wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.

**35.**-(1) Uwekezaji, riba au haki juu ya mali ambayo ni sehemu katika uwekezaji unaofanywa chini ya Sheria hii, hautachukuliwa na Serikali isipokuwa kwa maslahi ya umma.

(2) Endapo Serikali itachukuwa riba au haki juu ya mali ambayo ni sehemu katika uwekezaji chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mwekezaji atalipwa fidia inayostahiki na kwa wakati.

(3) Serikali haitachukua hatua au uamuzi wowote usiofaa ambao utaathiri haki au uwezo wa Mwekezaji kufanya kazi Zanzibar bila ya sababu halali na zinazokubalika.

Ulinzi wa haki miliki ya ubunifu.

**36.** Haki miliki za ubunifu za Mwekezaji zinazohusiana na Uwekezaji Ulioidhinishwa zitalindwa kwa mujibu wa sheria husika.

Ajira kwa Watanzania.

**37.** Mwekezaji ataajiri Watanzania kwa kuwapa kipaumbele Wazanzibari katika fani ambazo Watanzania au Wazanzibari wana sifa.

Ajira kwa wataalamu wa Kigeni.

**38.**-(1) Mwekezaji anaweza kuajiri wataalamu wa kigeni mpaka asilimia kumi ya wafanyakazi wote kwa kipindi cha miaka minane isipokuwa iwe imeelezwa vyenginevyo na sheria husika.

(2) Mwekezaji hatoajiri mtaalamu wa kigeni isipokuwa pale ambapo hakuna Mtanzania au Mzanzibari mwenye sifa zinazohitajika katika nafasi hiyo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka inaweza, baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mwekezaji, kuongeza idadi ya wataalamu wa kigeni na kipindi cha ukaazi wao baada ya kushauriana na mamlaka husika.

## SEHEMU YA SITA
## UTENGAJI WA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI

Utengaji wa Maeneo Maalumu ya Uchumi.

**39**.-(1) Kutakuwa na Maeneo Maalumu ya Uchumi ambayo yatajumuisha Maeneo ya Bandari Huru, Maeneo Huru ya Uchumi, Ardhi ya Akiba kwa Uwekezaji, Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya kusafirisha nje ya Nchi, Maeneo Huru ya Digitali, Maeneo Huru ya Viwanda, Maeneo ya Visiwa vidogo, Maeneo Huru ya Biashara, Maeneo ya Lojistiki na Vituo vya Mikutano.

(2) Rais anaweza, kwa tangazo lililochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutenga eneo lolote lililopo Zanzibar kuwa ni Eneo Maalumu la Uchumi na kuainisha mipaka, vivutio na msimamizi wake akiwa ni wa umma au binafsi;

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, Mamlaka itakuwa na uwezo wa kipekee wa udhibiti na usimamizi wa Maeneo Maalumu ya Uwekezaji isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Madhumuni ya Maeneo Maalumu ya Uchumi.

**40**. Madhumuni ya Maeneo Maalumu ya Uchumi ni:

(a) kuweka mazingira mazuri ya uendeshaji na kuwahakikishia maeneo ya uhakika ya biashara kwa Wawekezaji ikijumuisha:

(i) uendelezaji wa miundombinu jumuishi;

(ii) uwekaji wa vivutio kwa ajili ya shughuli za kibiashara na uchumi; na

(iii) uondoshaji wa vikwazo vya shughuli za uwekezaji na kibiashara;

(b) kurahisisha maendeleo ya kiteknolojia katika ujuzi maalumu na kuongeza uzalishaji kwa mauzo ya nje ya nchi;

(c) kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa Uwekezaji; na

(d) kuvutia huduma za kimataifa.

Kazi za Mamlaka katika Maeneo Maalumu ya Uchumi.

**41**. Mamlaka, kuhusiana na Maeneo Maalumu ya Uchumi:

(a) itatangaza sera na miongozo yote muhimu kwa ufanisi wa shughuli za uwekezaji;

(b) itatenga maeneo ya kijiografia yaliyotambuliwa ambayo yanafaa kwa uendelezaji wa uwekezaji kwa kuzingatia sera na sheria za ardhi za Zanzibar;

(c) itaainisha aina tofauti ya Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(d) itaainisha aina za huduma na biashara zinazoweza kuwemo katika maeneo hayo;

(e) itatoa, itapitia na itafuta leseni ya kuendeleza, kuendesha na kudumisha shughuli za uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi; na

(f) itafuatilia na itadhibiti shughuli za uwekezaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha na rasilimali za Mamlaka.

**42**. -(1) Fedha na rasilimali za Mamlaka zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zilizopokelewa kutokana na huduma zilizotolewa na Mamlaka;

(c) ruzuku, zawadi, misaada, michango au mikopo inayoweza kupokelewa kihalali na Mamlaka kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;

(d) mapato yanayotokana na uwekezaji wa Mamlaka; na

(e) fedha nyengine yoyote ambayo inaweza kumilikiwa au kupatikana kihalali na Mamlaka ikiwa kwa ufanyaji wa shughuli zake au vyenginevyo.

(2) Miamala yote ya kifedha ya Mamlaka itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

(3) Mamlaka itabakiza asilimia mia moja (100%) ya fedha ilizozikusanya.

Bajeti ya Mamlaka.

**43**.-(1) Mkurugenzi Mtendaji, katika kila mwaka wa fedha husika, ataandaa na kuwasilisha kwa Bodi kwa majadiliano na mapendekezo ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Mamlaka itashughulikiwa katika namna sawa kama ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Mamlaka yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na maelekezo mengine yoyote yatakayotolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mtendaji atahakikisha kwamba, malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Mamlaka ni sahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unadumishwa juu ya mali na madeni ya Mamlaka.

Hesabu na Ukaguzi.

**44**.-(1) Mamlaka itaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yake na kuhakikisha kwamba, fedha zote zilizopokelewa na kulipwa na Mamlaka zinasimamiwa, zinaidhinishwa na kudhibitiwa vizuri dhidi ya mali na madeni yake.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Mamlaka zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam.12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha zinazohusika.

Akaunti ya Benki.

**45**.-(1) Mwekezaji atafungua akaunti ya benki ya fedha za Kitanzania au fedha za kigeni katika benki yoyote iliyopo Zanzibar na atafanya miamala yote ya uwekezaji kupitia akaunti hiyo.

(2) Mwekezaji atafungua akaunti kwenye benki yoyote nje ya Zanzibar baada ya kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Mamlaka.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**46**. Mwekezaji ambaye:

(a) ametoa taarifa za uongo au upotoshaji kwa Mamlaka;

(b) amekataa au anadharau kutoa taarifa ambayo Mamlaka inaweza kuitaka kwa madhumuni ya kutekeleza masharti ya Sheria hii;

(c) amemzuia afisa yeyote wa Mamlaka kutekeleza majukumu yake halali aliyopewa chini ya Sheria hii; au

(d) amefungua akaunti ya benki nje ya Tanzania inayohusiana na Uwekezaji Uliyoidhinishwa bila ya ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mamlaka,

ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Dola za Kimarekani Elfu Hamsini au inayolingana na hiyo kwa Shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka miwili au adhabu zote mbili faini na kifungo.

Adhabu ya jumla.

**47**. Mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii, ambapo hakuna adhabu maalumu iliyowekwa kwa kosa hilo, ametenda kosa na, akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Dola za Kimarekani Elfu Kumi au inayolingana na hiyo kwa Shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua mwaka moja au adhabu zote mbili faini na kifungo.

Kumaliza kosa.

**48**.-(1) Mkurugenzi Mtendaji anaweza kumaliza kosa lililofanywa na Mwekezaji chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, iwapo Mwekezaji huyo:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa na atachukua tahadhari kwa kutorudia tena kosa; na

(b) atalipa malipo yote ya msingi chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hautochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka kwa kosa linaloshughulikiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

## SEHEMU YA TISA
## MASHARTI MENGINEYO

Kutambua makubaliano baina ya nchi mbili.

**49**. Kwa kuzingatia masharti ya sheria zinazohusika, mamlaka husika itazingatia makubaliano baina ya nchi mbili au zaidi yanayohusiana na uwekezaji ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia au ni sehemu ya makubaliano hayo.

Kutunza siri.

**50**. Bila ya kujali masharti ya sheria nyengine yoyote, taarifa zitakazotolewa na Mwekezaji zitakuwa siri kwa Mamlaka na hazitatolewa isipokuwa:

(a) kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii;

(b) kwa ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mwekezaji husika;

(c) endapo itahitajika kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria; au

(d) endapo itahitajika kutolewa kwa amri ya Mahakama.

Sifa na Vivutio vya Mnunuzi.

**51**. Mnunuzi ambaye amekidhi vigezo vilivyoanishwa katika kanuni, atastahiki kupata vivutio vilivyoainishwa chini ya Sehemu ya Nne ya Jadweli la Tano la Sheria hii.

Nyumba za biashara.

**52**. Mamlaka itashajiisha na kuidhinisha miradi ya nyumba za biashara kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

Daftari la Kumbukumbu.

**53**.-(1) Kutakuwa na daftari la kumbukumbu ambalo litajumuisha taarifa zote za Cheti cha Uwekezaji na taarifa nyengine zozote za Mwekezaji kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(2) Daftari la kumbukumbu litakuwa chini ya usimamizi wa Mkurugezi Mtendaji.

(3) Endapo Mwekezaji anakusudia kubadilisha taarifa zake, atatoa taarifa kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya mabadiliko hayo.

(4) Mkurugenzi Mtendaji, ndani ya siku saba za kazi kuanzia tarehe ya kupokea taarifa za mabadiliko na baada ya Mwekezaji kulipa ada iliyoainishwa chini ya kanuni, atafanya mabadiliko ya taarifa kwa mujibu wa taarifa alizopokea kutoka kwa Mwekezaji.

Kampuni ya Uendeshaji.

**54**.-(1) Uwekezaji Ulioidhinishwa unaweza kusimamiwa na Kampuni ya Uendeshaji baada ya kupata idhini ya maandishi na kulipa ada iliyoainishwa katika kanuni;

(2) Kampuni ya Uendeshaji iliyoidhinishwa kusimamia Uwekezaji Ulioidhinishwa itawezeshwa kupata kibali cha kazi na ukaazi na haitostahili kupatiwa Cheti cha Uwezekaji na vivutio vinavyotolewa chini ya Sheria hii.

(3) Taratibu za maombi ya uendeshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa zitaainishwa katika kanuni.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Kampuni ya Uendeshaji maana yake ni kampuni iliyosajiliwa Zanzibar kwa madhumuni makuu ya kusimamia na kuendesha Uwekezaji maalumu Ulioidhinishwa.

Uhaulishaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa.

**55**.-(1) Mwekezaji ambaye anakusudia kuhaulisha au kuondosha uwekezaji au hisa katika kampuni, maslahi au haki katika sehemu ya uwekezaji au uwekezaji wote, ataomba ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mamlaka kabla hajakamilisha uhaulishaji au uondoshaji huo na baada ya kulipa ada iliyoainishwa katika kanuni.

(2) Taratibu za maombi ya uhaulishaji au uondoshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa zitaainishwa katika kanuni.

Huduma za kielektroniki.

**56**. Bila ya kujali masharti ya Sheria hii au kanuni zake, Mamlaka, kwa njia za kielektroniki:

(a) itaidhinisha hatua za maombi na uamuzi wa utoaji wa Cheti cha Uwekezaji, kibali na leseni;

(b) itaidhinisha ulipaji wa ada yoyote iliyoainishwa; au

(c) itaelekeza utendaji wa jambo lolote linalotakiwa kufanywa chini ya Sheria hii au kanuni.

Utatuzi wa migogoro.

**57**.-(1) Endapo mgogoro utatokea baina ya Mwekezaji na Mamlaka au Serikali kuhusiana na uwekezaji, mgogoro huo utatatuliwa kwa njia ya maelewano.

(2) Mgogoro baina ya Mwekezaji na Mamlaka au Serikali ambao utakuwa haujasuluhishwa kupitia majadiliano unaweza kuwasilishwa kwa usuluhishi kwa mujibu wa:

(a) taratibu zilizoainishwa chini ya sheria inayosimamia Usuluhishi Zanzibar;

(b) kanuni za usuluhishi za Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Migogoro ya Uwekezaji; au

(c) ndani ya makubaliano yoyote baina ya nchi mbili au zaidi kuhusu kinga za uwekezaji yaliyosainiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi anayotoka mwekezaji.

Ada na tozo.

**58**. Ada na tozo zilizowekwa chini ya Sheria hii zitaainishwa katika kanuni.

Marekebisho ya Jadweli.

**59**.-(1) Kwa kuzingatia idhini ya Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Waziri anaweza kurekebisha, kubadilisha au kuongeza Jadweli lolote linalohusiana na vivutio vinavyotolewa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kurekebisha Jadweli jengine lolote isipokuwa Jadweli lililotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Mapitio na Rufaa.

**60**.-(1) Mwekezaji ambaye ameathirika na uamuzi uliofanywa na Mamlaka anaweza, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya uamuzi huo, kuwasilisha malalamiko yake kwa Bodi kwa ajili ya mapitio.

(2) Endapo Mwekezaji hakuridhika na uamuzi uliofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, anaweza, ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya uamuzi huo, kukata rufaa kwa Waziri.

(3) Waziri atafanya uamuzi wa maombi hayo ya rufaa kwa mujibu wa taratibu zilizoanishwa katika kanuni.

Kanuni.

**61**. Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**62**.-(1) Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litaendelea na litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

---

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 14]**

---

Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

**1.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Vikao vya Bodi.

**2.**-(1) Bodi itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana kwa kikao cha dharura muda wowote inapohitajika.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe waliokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**3.** Akidi ya vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wake.

Uamuzi ya Bodi.

**4.** Uamuzi ya Bodi utafanywa kwa makubaliano, ikiwa hakuna makubaliano, uamuzi utafanywa kwa wingi wa kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**5.** Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Taratibu za vikao.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itaandaa taratibu zake wenyewe za vikao.

Mjumbe mualikwa.

**7.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

**8.**-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusiana au linalotaka kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada ya kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi hayo:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; au

(b) hatomshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**9**. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) kujiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu ya msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasitishwa na Waziri akishindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka;

(e) ikiwa amehukumiwa kifungo kwa kipindi cha miezi sita au zaidi; au

(f) kifo.

Posho za wajumbe.

**10**. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi wanastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam.2 ya 2011 na sheria nyengine zinazohusika.

Kamati za Bodi.

**11**.-(1) Bodi inaweza kuanzisha kamati kwa madhumuni ya kutekeleza kazi maalumu kama itakavyoona inafaa.

(2) Wajumbe wa kamati watakuwa ama ni miongoni mwa wajumbe wa Bodi au wajumbe wengine watakaoteuliwa na Bodi.

**JADWELI LA PILI**

**MTAJI WA UWEKEZAJI**
**[Chini ya kifungu cha 24 na 25]**

---

## SEHEMU YA KWANZA
## MTAJI WA UWEKEZAJI

1. Maombi ya Cheti cha Uwekezaji yatazingatiwa iwapo asilimia mia moja ya hisa za Kampuni zinamilikiwa na:

   (a) Mtanzania na mtaji wa uwekezaji usiopungua Dola za Kimarekeni Laki Moja;

   (b) Diaspora na mtaji wa uwekezaji usipoungua Dola za Kimarekani Laki Mbili;

   (c) Mwekezaji wa Kigeni au inayomilikiwa kwa ubia na Mtanzania na mtaji wa uwekezaji usiopungua Dola za Kimarekani Milioni Mbili na Laki Tano kwa miradi ya Uwekezaji wa Hoteli na Ujenzi wa Nyumba za Biashara; au

   (d) Mwekezaji wa Kigeni au inayomilikiwa kwa ubia na Mtanzania na mtaji wa uwekezaji usiopungua Dola za Kimarekani Laki Tano kwa sekta nyengine ya miradi ya uwekezaji.

## SEHEMU YA PILI
## VIGEZO VYA HADHI YA UWEKEZAJI MKAKATI

2. Uwekezaji Ulioidhinishwa Unguja utapewa hadhi ya Uwekezaji Mkakati ikiwa Mwekezaji amewekeza:

   (a) Dola za Kimarekani Milioni Hamsini kwa Mwekezaji wa Kigeni au Mtanzania na kuchangia angalau asilimia thelathini ya mtaji uliowekezwa iwe kwenye mchango wa wanahisa;

   (b) Dola za Kimarekani Milioni Kumi na kutengeneza angalau ajira mia tano za moja kwa moja kwa Watanzania katika sekta nyengine zisizokuwa za hoteli;

   (c) katika visiwa vidogo vidogo chini ya masharti ya Sheria hii.

3. Uwekezaji Ulioidhinishwa Pemba utapewa hadhi ya Uwekezaji Mkakati iwapo Mwekezaji amewekeza:

(a) Dola za Kimarekani Milioni Tano kwa Mwekezaji wa Kigeni au Mtanzania na kuchangia angalau asilimia thelathini ya mtaji uliowekezwa uwe kwenye mchango wa wanahisa.

(b) Dola za Kimarekani Milioni Mbili na kutengeneza angalau ajira mia moja za moja kwa moja kwa Watanzania katika sekta nyengine zisizokuwa za hoteli;

(c) katika visiwa vidogo vidogo chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA TATU

## VIVUTIO VYA WAWEKEZAJI WALIOIDHINISHWA NJE YA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI

**[Chini ya kifungu cha 26]**

---

## SEHEMU YA KWANZA
## VIVUTIO WAKATI WA KIPINDI CHA UTEKELEZAJI

**1.** Mwekezaji ambaye anawekeza nje ya Maeneo Maalumu ya Uchumi, anaweza kupatiwa vivutio vifuatavyo:

(a) asilimia Sabini na Tano ya msamaha wa ushuru na kodi ya uingizaji wa vifaa vya ujenzi au vifaa vinavyohitajika kabla ya uendeshaji na bidhaa nyengine zozote zenye asili ya mtaji;

(b) asilimia Mia Moja ya msamaha wa ushuru na kodi katika manunuzi ya ndani ya vifaa vya ujenzi au bidhaa zinazohitajika kabla ya uendeshaji wa mradi na bidhaa nyengine zozote zenye asili ya mtaji;

(c) asilimia Hamsini ya msamaha wa kodi ya mapato kwa riba ya mtaji uliokopwa kutoka benki za kigeni;

(d) msamaha wa kodi ya ukodishwaji ardhi kwa muda usiozidi mwaka mmoja kuanzia tarehe ya ukodishwaji ardhi;

(e) asilimia Mia Moja ya umiliki wa kigeni unaruhusiwa;

(f) kuwatumia wakandarasi wa kigeni inaruhusiwa, kwa sharti kwamba, vifaa na mashine zote za ujenzi zitakuwa chini ya mpango wa muda wa uingizaji; na

(g) msamaha wa kodi ya matumizi ya ardhi ya baharini kwa mwaka mmoja kuanzia tarehe ya ukodishwaji ardhi.

## SEHEMU YA PILI
## VIVUTIO WAKATI WA UENDESHAJI

2. Mwekezaji ambaye anawekeza nje ya Maeneo Maalumu ya Uchumi anaweza kupewa vivutio vifuatavyo;

(a) kwa maombi, msamaha wa asilimia Mia Moja wa kodi ya mapato inayopaswa kulipwa na kampuni kwa miaka mitano ya kwanza;

(b) msamaha wa asilimia Mia Moja wa kodi inayotokana na uchakavu wa vitu kwa miaka mitano;

(c) msamaha wa asilimia Mia Moja katika kazi za utafiti na maendeleo kwa miaka mitano; na

(d) ruhusa ya kubakiza asilimia Mia Moja ya faida baada ya malipo ya kodi.

## SEHEMU YA TATU
## SEKTA YA UZALISHAJI

3. Bila ya kuathiri masharti ya Sehemu ya Kwanza na ya Pili ya Jadweli hili, Mwekezaji ambaye amewekeza katika sekta ya uzalishaji anaweza kupewa vivutio vya ziada vifuatavyo:

(a) msamaha wa asilimia Mia Moja wa kodi yoyote kwa bidhaa zote zinazozalishwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi;

(b) msamaha wa asilimia Mia Moja wa ushuru, ada au tozo nyengine zozote kwa malighafi na pembejeo za viwandani zinazonunuliwa kutoka Tanzania Bara;

(c) msamaha wa asilimia Mia Moja wa ushuru wa uingizaji, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine zinazofanana kwa malighafi na bidhaa za vifungashio;

(d) punguzo la uingizaji wa malighafi na pembejeo za viwandani zinazotolewa chini ya Sheria za forodha za Jumuiya ya Africa Mashariki kwa kuzingatia maombi yatakayofanywa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(e) msamaha wa asilimia Mia Moja wa Kodi ya Mapato kwa mtaji uliokopwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa uendeshaji.

## JADWELI LA NNE

## VIVUTIO VYA UWEKEZAJI MKAKATI
**[Chini ya kifungu cha 26]**

---

## SEHEMU YA KWANZA
## VIVUTIO KIPINDI CHA UTEKELEZAJI WA MRADI

1. Mwekezaji ambaye amepatiwa hadhi ya Uwekezaji Mkakati anaweza kupatiwa vivutio vifuatavyo:

   (a) kwa maombi, msamaha wa asilimia Mia Moja wa ushuru na kodi ya uingizaji na manunuzi ya ndani ya vifaa vya ujenzi au vifaa vinavyohitajika kabla ya uendeshaji na bidhaa nyengine zozote zenye asili ya mtaji;

   (b) msamaha wa asilimia Mia Moja wa Kodi ya Mapato kwa riba ya mtaji uliokopwa kutoka benki za kigeni;

   (c) msamaha wa kodi ya matumizi ya ardhi kwa miaka isiyozidi mitano kuanzia tarehe ya ukodishwaji ardhi;

   (d) asilimia Mia Moja ya umiliki wa kigeni unaruhusiwa;

   (e) kuwatumia wakandarasi wa kigeni inaruhusiwa, kwa sharti kwamba, vifaa na mashine zote za ujenzi zitakuwa chini ya mpango wa muda wa uingizaji;

   (f) msamaha wa kodi ya matumizi ya ardhi ya baharini kwa miaka mitano kuanzia tarehe ya ukodishwaji ardhi; na

   (g) msamaha wa asilimia Mia Moja wa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika huduma za ujenzi kwa Pemba na katika visiwa vidogo vidogo ndani ya Zanzibar.

## SEHEMU YA PILI
## VIVUTIO KIPINDI CHA UENDESHAJI

**2.** Mwekezaji ambaye amepatiwa hadhi ya Uwekezaji Mkakati, anaweza, itakapoonekana inafaa, kupatiwa vivutio vifuatavyo wakati wa uendeshaji wa Uwekezaji Ulioidhinishwa:

(a) kwa maombi, msamaha wa asilimia Mia Moja wa kodi ya mapato inayopaswa kulipwa na kampuni kwa miaka mitano ya kwanza na msamaha wa asilimia Hamsini kwa kipindi cha miaka kumi inayofuata;

(b) ruhusa ya asilimia Mia Moja ya kuhamisha faida ya tawi;

(c) msamaha wa asilimia Mia Moja ya kodi inayotokana na uchakavu wa mitambo na mashine kwa kipindi cha miaka mitano;

(d) msamaha wa asilimia Mia Moja katika kazi ya utafiti na maendeleo kwa miaka mitano; na

(e) ruhusa ya kubakiza asilimia Mia Moja ya faida baada ya kulipa kodi zote zinazohusika.

## SEHEMU YA TATU
## SEKTA YA UZALISHAJI

**3.** Bila kuathiri masharti ya Sehemu ya Kwanza na ya Pili ya Jadweli hili, Mwekezaji ambaye amepatiwa hadhi ya Uwekezaji Mkakati aliyewekeza katika sekta ya uzalishaji anaweza kupewa vivutio vya ziada vifuatavyo:

(a) msamaha wa asilimia Mia Moja wa kodi yoyote kwa bidhaa zote zinazozalishwa kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi;

(b) msamaha wa asilimia Mia Moja wa ushuru, ada au tozo nyengine yoyote kwa malighafi na pembejeo za viwandani zilizonunuliwa kutoka Tanzania Bara;

(c) msamaha wa asilimia Mia Moja wa malipo ya ushuru wa uingizaji, ushuru wa bidhaa na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa uingizaji wa zana na mashine nzito;

(d) msamaha wa asilimia Mia Moja wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ununuzi wa ndani wa vifaa na mashine nzito zinazohitajika katika kipindi cha uzalishaji;

(e) msamaha wa asilimia Mia Moja wa malipo ya ushuru wa uingizaji, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengineyo zinazofanana kwa malighafi na bidhaa za vifungashio vinavyohitajika kipindi cha uendeshaji wa mradi;

(f) punguzo la uingizaji wa malighafi na pembejeo za viwandani zinazotolewa chini ya Sheria za Forodha za Jumuiya ya Africa Mashariki kwa kuzingatia maombi yatakayofanywa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na

(g) msamaha wa asilimia Mia Moja wa Kodi ya Mapato kwa mtaji uliokopwa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka wa uendeshaji

## JADWELI LA TANO

## VIVUTIO VYA WAWEKEZAJI WALIOIDHINISHWA KATIKA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI

**[Chini ya kifungu cha 26]**

---

## SEHEMU YA KWANZA
## MWENDELEZAJI KATIKA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI

1. Mwendelezaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi anaweza kupewa vivutio vifuatavyo:

   (a) msamaha wa asilimia Sabini na Tano unaotokana na malipo ya kodi na ushuru wa mashine, vifaa, magari ya kazi nzito, vifaa vya ujenzi na bidhaa nyengine zozote zenye asili ya mtaji zitakazotumika kwa madhumuni ya kuendeleza miundombinu ya Maeneo Maalumu ya Uchumi;

   (b) msamaha unaotokana na malipo ya ushuru wa mapato ya kampuni kwa kipindi cha mwanzo cha miaka kumi;

   (c) msamaha unaotokana na malipo ya kodi ya zuio inayotokana na pango, gawio na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

   (d) msamaha unaotokana na malipo ya kodi ya mali kwa miaka kumi ya mwanzo;

   (e) punguzo la ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine yoyote inayotakiwa kulipwa kuhusiana na uingizaji nchini wa gari moja la utawala, gari la kubebea wagonjwa, zana na gari ya kuzimia moto na mabasi mpaka mawili kwa ajili usafiri wa wafanyakazi kuwapeleka na kuwarejesha katika Maeneo Maalumu ya Uchumi;

   (f) msamaha kutokana na malipo ya ushuru wa stempu kwa hati yoyote inayotekelezwa ndani au nje ya Maeneo Maalumu ya Uchumi inayohusiana na uhaulishaji au ukodishaji wa mali yoyote inayohamishika au isiohamishika iliyomo ndani ya Maeneo Maalumu ya Uchumi au waraka, Cheti cha Uwekezaji, hati, ripoti, taarifa au kumbukumbu yoyote inayohusiana na shughuli yoyote, kitendo, uendeshaji, mradi, utekelezaji au uwekezaji ndani ya Maeneo Maalumu ya Uchumi.

## SEHEMU YA PILI
## WAENDESHAJI NDANI YA MAENEO MAALUMU YA UCHUMI

**2.** Wawekezaji ambao mauzo yao ya msingi yanafanyika ndani ya eneo la Udhibiti wa Forodha watastahiki:

(a) punguzo la ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine yoyote inayotozwa kwa malighafi na bidhaa zenye asili ya mtaji zinazohusiana na uzalishaji katika Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(b) msamaha unaotokana na malipo ya kodi la zuio kwa riba ya mkopo wa kigeni kutoka taasisi za kifedha;

(c) punguzo la ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine yoyote inayotakiwa kulipwa kuhusiana na uingizaji nchini wa gari moja la utawala, gari la kubebea wagonjwa, zana na gari ya kuzimia moto na mabasi mpaka mawili kwa ajili ya usafiri wa wafanyakazi kuwapeleka na kuwarejesha katika Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(d) msamaha unaotokana na ukaguzi kabla ya kusafirisha au baada ya kuingia;

(e) ukaguzi wa kiforodha wa bidhaa ndani ya Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(f) kupata huduma zenye ushindani, za kisasa na za uhakika zinazopatikana ndani ya Maeneo Maalumu ya Uchumi;

(g) asilimia Mia Moja ya kupata soko la huduma na bidhaa kwa kuzingatia masharti ya forodha ya uingizaji katika mamlaka za forodha kama ilivyoanishwa chini ya sheria za Forodha za Jumuiya ya Afrika Mashariki; na

(h) kwa kuzingatia masharti na taratibu za ubadilishaji wa fedha za kigeni na malipo ya kodi pale inapofaa, uhamisho usio na masharti kupitia benki yoyote ya muuzaji iliyoidhinishwa kwa sarafu inayobadilishwa kwa uhuru wa:

   (i) faida inayopatikana au gawio lililotokana na uwekezaji;

   (ii) malipo yanayohusiana na huduma za mkopo endapo mkopo wa nje umepatikana;

   (iii) mrabaha, ada na tozo zinazohusiana na makubaliano ya ubadilishaji wa teknolojia;

(iv) utumaji wa mapato katika tukio la mauzo au kufutwa kwa biashara iliyoruhusiwa au riba yoyote inayotokana na biashara iliyoruhusiwa; na

(v) malipo ya mishahara na mafao mengine kwa wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa Tanzania wanaohusiana na biashara iliyoruhusiwa.

## SEHEMU YA TATU
## WAENDESHAJI NDANI YA MAENEO YA UZALISHAJI KWA AJILI YA KUSAFIRISHA NJE YA NCHI

3. Mwekezaji anayezalisha kwa ajili ya soko la nje katika eneo ambalo sio la viwanda au sekta ya uzalishaji atastahiki:

(a) kwa kuzingatia masharti na utaratibu unaotumika, kupata mpango wa dhamana ya mkopo wa usafirishaji nje;

(b) punguzo la ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine yoyote inayotozwa katika malighafi na bidhaa za vifungashio na bidhaa zenye asili ya mtaji zinazohusiana na uzalishaji katika Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Kusafirisha nje ya nchi;

(c) msamaha unaotokana na kodi ya mapato inayopaswa kulipwa na kampuni kwa miaka kumi ya kwanza;

(d) msamaha unaotokana na malipo ya kodi ya zuio inayotokana na ukodishaji, gawiyo na riba kwa miaka kumi ya mwanzo;

(e) msamaha unaotokana na malipo ya kodi zote na ushuru uliowekwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa bidhaa zinazozalishwa katika Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi kwa kipindi cha miaka kumi;

(f) msamaha unaotokana na ukaguzi kabla ya kusafirisha au baada ya kuingia;

(g) ukaguzi wa bidhaa ndani ya Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Kusafirisha nje ya nchi;

(h) punguzo la ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi nyengine yoyote inayotakiwa kulipwa kuhusiana na uingizaji nchini wa gari moja la utawala, gari la kubebea wagonjwa, zana za kuzimia moto na gari la kuzimia moto na mabasi mpaka mawili kwa ajili usafiri wa wafanyakazi kuwapeleka na kuwarejesha katika Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi;

(i) ushughulikiaji wa bidhaa zilizoingizwa ndani ya Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Kusafirisha nje ya nchi kama bidhaa za mpito;

(j) kupata huduma zenye ushindani za kisasa na za uhakika zinazopatikana ndani ya Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Kusafirisha nje ya nchi;

(k) kwa kuzingatia masharti na taratibu za ubadilishaji wa fedha za kigeni na malipo ya kodi, pale inapofaa, uhamisho usio na masharti kupitia benki yoyote ya muuzaji iliyoidhinishwa kwa sarafu inayobadilishwa kwa uhuru wa:

   (i) faida inayopatikana au gawio lililotokana na uwekezaji;

   (ii) malipo yanayohusiana na huduma za mkopo endapo mkopo wa nje umepatikana;

   (iii) mirabaha, ada na tozo zinazohusiana na makubaliano ya ubadilishaji wa teknolojia;

   (iv) utumaji wa mapato katika tukio la mauzo au kufutwa kwa biashara iliyoruhusiwa au riba yoyote inayotokana na biashara iliyoruhusiwa; na

   (v) malipo ya mishahara na mafao mengine kwa wafanyakazi wa kigeni walioajiriwa Tanzania wanaohusika na biashara iliyoruhusiwa;

(l) asilimia Ishirini ya mauzo yote yanaruhusiwa kuuzwa kwa soko la ndani na yatatozwa malipo ya kodi zote;

(m) asilimia Mia Moja ya umiliki wa kigeni unaruhusiwa; na

(n) hakuna ukomo wa muda ambao bidhaa zinaweza kuhifadhiwa katika Maeneo ya Uzalishaji kwa ajili ya Kusafirishwa nje ya nchi.

4. Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Mwekezaji aliyepewa leseni kwa ajili ya kusafirisha katika masoko ya nje ambayo mauzo yake ni zaidi ya asilimia Themanini ya jumla ya uzalishaji wa kila mwaka.

**SEHEMU YA NNE**
**MWENDELEZAJI NA MNUNUZI WA MIRADI YA NYUMBA ZA BIASHARA**

**5**. Mwendelezaji aliyewekeza katika miradi ya Nyumba za Biashara anaweza kupatiwa vivutio vifuatavyo:

(a) msamaha wa asilimia Mia Moja kutokana na malipo ya kodi ya zuio inayotokana na riba;

(b) Msamaha wa asilimia Mia Moja wa ushuru wa stempu kwa kila mkataba wa manunuzi;

(c) mkataba wa ukodishwaji ardhi ni miaka thelathini na tatu; na

(d) mkataba wa ukodishwaji ardhi ya baharini ni miaka thelathini na tatu.

**6**. Mnunuzi wa Nyumba katika Mradi wa Nyumba za Biashara yenye thamani isiyopungua Dola za Kimarekani Laki Moja anaweza kupewa vivutio vifuatavyo:

(a) kibali cha ukaazi kwa mnunuzi, mwenza wake na watoto wake wanne walio chini ya umri wa miaka ishirini;

(b) asilimia Hamsini ya msamaha wa ushuru wa stempu;

(c) umiliki wa asilimia Mia Moja wa kigeni unaruhusiwa; na

(d) kuhamisha asilimia Mia Moja ya faida inayotokana na mauzo baada ya kodi.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 4 Disemba, 2023.

..............................................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***